# GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

*(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)*

**Sehemu ya CXXXIII Nam. 7140** **23 Agosti, 2023** **Bei, Shs. 4,000**

*Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti*

**YALIYOMO** *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam. 11 ya 2003 ya Kutunga Sheria ya Ukaguzi wa Umma na Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo: ................................................ 481

## SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

### Tangazo la Mswada

Nam. :- Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam. 11 ya 2003 ya Kutunga Sheria ya Ukaguzi wa Umma na Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo: .

### TANGAZO

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 13 Septemba, 2023 kwa kusomwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

**ZANZIBAR**
23 Agosti, 2023

(Mhandisi Zena Ahmed Said)
***Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.***

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

**MSWADA**

*wa*

**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA KUANZISHA AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI, NAM. 11 YA 2003 NA KUTUNGA SHERIA YA UKAGUZI WA UMMA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2023 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais.

Matumizi.

**2.-**(1) Sheria hii itatumika kuhusiana na masuala ya ukaguzi wowote na taratibu nyengine chini ya mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yaliyoelezwa chini ya Katiba na sheria nyengine yoyote.

(2) Endapo sheria yoyote itakuwa inapingana na masharti ya Sheria hii, masharti ya Sheria hii yatakuwa na nguvu.

Ufafanuzi.

**3.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Afisa Masuuli" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016;

"Afisi" maana yake ni Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hii;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Utumishi ya Afisi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 23(1) cha Sheria hii;

"Hesabu za Umma" maana yake ni hesabu zote za taasisi za umma ambazo zinaweka kumbukumbu zote za fedha zilizopokelewa au zilizolipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina;

"Kanuni za Maadili na Utendaji" maana yake ni Kanuni za Maadili na Utendaji zilizotungwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali chini ya Sheria hii;

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Zanzibar ya 1984;

"Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali" maana yake ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 112 cha Katiba;

"Mfuko Mkuu wa Hazina" maana yake ni Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali uliotajwa chini ya kifungu cha 104(1) cha Katiba;

"Mkaguliwa" maana yake ni taasisi ya umma au chombo chengine chochote kinachokaguliwa chini ya Sheria hii;

"Mkaguzi" maana yake ni mkaguzi aliyeajiriwa chini ya kifungu cha 17(1) cha Sheria hii;

"Mlipaji Mkuu wa Serikali" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016;

"Mwaka wa Fedha" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Rasilimali" inajumuisha fedha, ghala, vifaa, mali, huduma za mikopo, wafanyakazi, uwekezaji na mali nyengine ambazo zinaweza kutumiwa na mtu au taasisi kwa ajili ya kufanya kazi kwa ufanisi;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Taasisi ya Umma" inajumuisha wizara, idara, wakala, mamlaka za serikali za mitaa, mashirika ya umma na chombo chengine chochote cha umma kilichoanzishwa kwa mujibu wa sheria;

"Udhibiti wa Ndani" maana yake ni seti ya mifumo iliyowekwa kuhakikisha kwamba kumbukumbu za fedha na nyenginezo zinaaminika, kamili na kuhakikisha zinaendana na usimamizi wa sera za taasisi;

"Ukaguzi wa kiuchunguzi" maana yake ni ukaguzi unaokusudia kubaini na kuzuia kutokufuata taratibu, kama vile udanganyifu, ubadhirifu, matumizi mabaya ya fedha au rushwa na matumizi ya ujuzi wa ukaguzi kwa hali ambazo zina athari za kisheria;

"Ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA" maana yake ni uchunguzi wa udhibiti unaohusiana na mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili kupata usahihi na kubaini kama mifumo hiyo inalinda mali, inaweka usiri, uadilifu na upatikanaji wa taarifa zinazohusiana na taasisi za umma;

"Utaratibu wa usimamizi" maana yake ni utaratibu wa usimamizi ulioanzishwa na Kamati za Hesabu za Umma za Baraza la Wawakilishi;

"Viwango vya Ukaguzi" maana yake ni viwango vya ukaguzi vilivyotolewa na Taasisi za Ukaguzi na Uhasibu za ndani au Kimataifa kama ilivyoamuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na ukaguzi.

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHWAJI WA AFISI

Uanzishwaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**4.-**(1) Kunaanzishwa Afisi itakayojulikana kama Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kwa ufupisho wake utakuwa ni OCAGZ.

(2) Afisi itakuwa ni chombo kinachojitegemea chenye kurithiwa na kwa jina lake, itakuwa na uwezo wa:

(a) kushtaki na kushtakiwa;

(b) kupata, kumiliki na kuondosha mali yoyote inayohamishika na isiyohamishika;

(c) kuingia katika mkataba au muamala wowote kwa mujibu wa sheria;

(d) kukopa kiwango chochote cha fedha kutoka taasisi za fedha zozote kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016; na

(e) kutekeleza au kufanya jambo au kitu chochote ambacho Afisi kwa uasili wake, inaweza kwa mujibu wa sheria kukitekeleza au kukifanya.

Muhuri.

**5.-**(1) Afisi itakuwa na muhuri ambao utawekwa chini ya dhamana ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au afisa mwengine yeyote wa Afisi kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakavyoelekeza.

(2) Matumizi ya muhuri wa Afisi katika waraka mwengine wowote yatathibitishwa na saini ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au Afisa mwengine wa Afisi aliyeidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(3) Waraka wowote unaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Afisi utawekwa muhuri wa Afisi na utathibitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Kazi za Afisi.

**6.** Afisi itatekeleza kazi, majukumu na uwezo wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyoainishwa chini ya Katiba, Sheria hii au sheria nyengine yoyote.

Uhuru wa Afisi.

**7.-**(1) Afisi itafanya kazi zake kwa haki, bila ya woga, upendeleo au kuathiriwa na itatekeleza uwezo wake kwa uhuru kwa mujibu wa masharti ya Katiba, Sheria hii na sheria nyengine yoyote.

(2) Uhuru wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulioainishwa chini ya kifungu cha 112(7) cha Katiba utatumika sawa kwa Afisi.

Muundo wa Utumishi wa Afisi.

**8.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011, Afisi itakuwa na Muundo wa Utumishi kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi na majukumu ya Afisi.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI WA AFISI

Uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**9.-**(1) Kwa kuzingatia masharti ya Katiba, kutakuwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakayeteuliwa na Rais.

(2) Wakati wa uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Rais, pamoja na sifa zilizoainishwa chini ya kifungu cha 112(2) cha Katiba, anaweza kuzingatia sifa husika za kitaaluma, uzoefu na ujuzi.

(3) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yake, atakula kiapo mbele ya Rais.

Mamlaka ya Kikatiba.

**10.-**(1) Mamlaka ya Kikatiba ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yatakuwa kama yalivyoainishwa katika kifungu cha 112(3) cha Katiba.

(2) Bila ya kuathiri Mamlaka ya Kikatiba chini ya kifungu cha 112(3) cha Katiba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakagua na kuripoti juu ya hesabu, taarifa za fedha na usimamizi wa fedha wa taasisi za umma na miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo.

Kuondolewa madarakani.

**11.** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kuondolewa madarakani kwa sababu na taratibu kama ilivyoainishwa chini ya kifungu cha 113 cha Katiba.

Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**12.-**(1) Pamoja na kazi alizopewa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizoainishwa katika Katiba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, atakuwa na jukumu la:

(a) kuchunguza, kuhoji, kukagua na kuripoti hesabu za:

(i) taasisi zote za umma au chombo cha umma ambacho kinapokea fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina au kutokana na fedha za umma kwa madhumuni ya umma; na

(ii) watu wote waliopewa dhamana ya kukusanya, kupokea, kusimamia, kutoa au kufanya malipo ya fedha za umma kwa stakabadhi, mauzo, uhaulishaji au utoaji wa stempu, dhamana, ghala au mali nyengine za umma; na

(b) kufanya ukaguzi mwengine wowote kama ilivyoainishwa na Sheria hii au sheria nyengine.

(2) Katika kutekeleza majukumu chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atahakikisha kuwa:

(a) hesabu zote zimewekwa kwa mujibu wa misingi ya jumla ya uhasibu inayokubalika;

(b) tahadhari zote muhimu zimechukuliwa kulinda, ukusanyaji na upokeaji wa mapato, uuhifadhi, uondoshaji, utoaji na ufanyaji wa matumizi sahihi ya mali za umma na kwamba sheria, maagizo na maelekezo yanayotumika yamezingatiwa kikamilifu;

(c) fedha zote za matumizi ya umma yameidhinishwa kwa usahihi na yametumika kwa madhumuni yaliyoidhinishwa na kwamba sheria, maagizo na maelekezo yanayotolewa yamezingatiwa ipasavyo na kutoa uangalizi bora wa tathmini na ukusanyaji wa mapato; na

(d) matumizi ya rasilimali za umma yametumika kwa kuzingatia uchumi, ubora na ufanisi.

(3) Kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake kama zilivyoelezwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kumpangia muajiriwa yoyote wa Afisi katika taasisi yoyote ya umma kutekeleza majukumu kwa ufanisi, na taasisi hiyo itampatia mahitaji muhimu ya kiofisi.

Uwezo wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**13.-**(1) Katika kutekeleza kazi na majukumu yake, Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, anaweza:

(a) kumuita afisa wa umma yeyote kwa ajili ya kutoa maelezo na taarifa zozote ambazo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kuzihitaji ili kumuwezesha kutekeleza kazi na majukumu hayo ipasavyo;

(b) kumuita na kumchunguza mtu yeyote kama atakavyoamua kuhusiana na upokeaji na matumizi ya fedha za umma au kupokea au kutoa mali yoyote ya umma iliyoathirika masharti ya Sheria hii na kuhusiana na jambo lolote muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake;

(c) kumuidhinisha mtu yeyote mwenye sifa ya kuteuliwa kama mkaguzi kufanya mahojiano, uchunguzi au ukaguzi kwa niaba yake na mtu huyo ataripoti kwake;

(d) bila malipo ya ada yoyote, atawezesha kufanyika upekuzi katika, na kuchukuliwa sehemu ya taarifa kutoka kwenye kitabu, nyaraka au kumbukumbu yoyote katika taasisi yoyote ya umma au taasisi nyengine yoyote;

(e) kukubali cheti cha mtu mwengine yeyote kama anavyoona inafaa kama ni halisi na sahihi bila ya kufanywa uchunguzi wa ziada, au kutegemewa kwenye hesabu ya mtu mwengine yoyote aliyepewa dhamana ya kukusanya, kupokea,

kutunza, kudhibiti au kulipa fedha za umma au mali ya umma au kwa kutoa, kuuza, kuhamisha au kuwasilisha mali ya umma; na

(f) kupata huduma za mtu yeyote kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 20 cha Sheria hii.

(2) Katika kutathmini na kuchunguza hatua na taratibu za manunuzi ya umma, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, anaweza kutumia matokeo ya zabuni kama ni muongozo wa kufikia hitimisho endapo ni muhimu katika kutekeleza kazi zake.

(3) Endapo wakati wowote itatokea kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba:

(a) malipo yoyote yamefanywa bila ya kuidhinishwa kwa mujibu wa sheria;

(b) kosa lolote imetokea katika kupokea, kuhifadhi, kudhibiti, kutoa, kuhamisha au kuwasilisha mali yoyote ya umma;

(c) upungufu wowote au upotevu uliosababishwa kwa uzembe, ukosefu wa maadili, udanganyifu au rushwa imetokea;

(d) kutokea kushindwa kufuata misingi ya uhifadhi kwa kiwango kikubwa; au

(e) kiwango chochote ambacho kilichopaswa kuwepo au hakijaingizwa katika hesabu,

kwa upande wa matumizi ya Serikali, Mahakama au Baraza la Wawakilishi, hatoruhusu matumizi hayo kama tozo ya fedha za umma na ataita kuhoji kiwango cha fedha zinazohusika.

(4) Endapo masuala yoyote yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, yanahusiana na matumizi ya Serikali, Mahakama au Baraza la Wawakilishi, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha kwa Rais kila ripoti atakayoandaa na masharti ya kifungu cha 112(5) cha Katiba yatatumika kwa kila ripoti hiyo.

(5) Katika kila jambo ambalo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataliandalia ripoti chini ya kifungu hiki, atamjuulisha Mlipaji Mkuu au Afisa Masuuli au mamlaka husika, ikiwa itakuwa ni sahihi kwamba mtu aliyehusika katika matumizi ya fedha za umma au mali inayohusiana na jambo lolote katika kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, alipe hasara au upotevu uliotokea na hatua za kinidhamu, malipo ya ziada, hatua za kisheria au hatua zote kwa pamoja zichukuliwe dhidi ya muhusika.

(6) Katika kutekeleza uwezo wake, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu mwengine yeyote aliyemuidhinisha kwa maandishi atakuwa na uwezo wa kupata taarifa kama ilivyoainishwa chini ya kifungu cha 15 ya Sheria hii.

(7) Kwa kuzingatia jukumu lolote alilopewa na sheria yoyote, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuwa na mamlaka kamili katika kutekeleza majukumu yake, na mahasus, katika kuamua endapo kufanya uchunguzi chini ya Sehemu ya Tano ya Sheria hii na kwa namna ambayo uchunguzi huo utafanyika.

Uwezo wa kutoa mapendekezo.

**14.** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza, kwa madhumuni ya:

(a) kuzuia au kupunguza matumizi ya fedha za umma yasiyo na tija;

(b) kuongeza ukusanyaji wa mapato ya serikali;

(c) kusimamia mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano kutokana na viashiria hatarishi vilivyopo kuhusiana na usiri, uadilifu na upatikanaji wa taarifa;

(d) kuzuia upotevu unaosababishwa na uzembe, kutokujali, wizi, kutokuwa na uaminifu, udanganyifu au rushwa inayohusiana na fedha na rasilimali za umma;

(e) kuzuia utakatishaji wa fedha haramu;

(f) kujengewa uwezo kwa taasisi; au

(g) kufuata taratibu zilizowekwa katika utekelezaji wa majukumu kwa taasisi,

kupendekeza kwa Waziri husika au Mkuu wa taasisi kama atakavyoona inafaa kwa ajili ya usimamizi bora wa fedha na rasilimali za umma ikijumuisha mapitio ya sheria.

Uwezo wa kupata taarifa.

**15.-**(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu aliyeidhinishwa na yeye atakuwa na uwezo bila ya vikwazo, wa kupata taarifa kutoka kwa mtu, nyaraka, kompyuta, mifumo ya taarifa na mali kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakavyoona ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi, majukumu na uwezo wake.

(2) Afisa Masuuli wa Mkaguliwa atahakikisha kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anapata nyaraka zinazohusiana na utekelezaji wa kazi, majukumu na uwezo wake muda wote unaofaa.

(3) Bila ya kujali sheria nyengine yoyote, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuwa na haki ya kupata nakala ya ripoti ya ukaguzi yoyote iliyoandaliwa katika taasisi za umma.

(4) Kwa madhumuni ya kutekeleza kazi, majukumu na uwezo wake, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kumtaka Mkaguliwa au mtu aliyeajiriwa na Mkaguliwa:

(a) kuwasilisha nyaraka yoyote au hati iliyo katika uhifadhi, uangalizi au udhibiti wa Mkaguliwa au mtu mwengine; na

(b) kumpatia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali taarifa au maelezo kuhusiana na taarifa, mfumo au mali yoyote.

(5) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kupata taarifa kama atakavyoona inafaa katika kukamilisha utekelezaji wa kazi, majukumu na uwezo wake, kutoka kwa mtu yeyote ambaye sio muajiriwa au afisa wa Mkaguliwa na katika kufanya hivyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza:

(a) kumshauri mtu kwa maandishi uhalisia wa taarifa na sababu za kuhitajika kwake;

(b) kuelezea kwamba taarifa zinahitajika chini ya Sheria hii;

(c) kutaka taarifa za ziada endapo itakuwa ni muhimu;

(d) kumwita mtu, ikiwa atahitajika; au

(e) kumrejeshea mtu gharama alizotumia wakati wa kusafiri endapo mtu huyo ameitwa kuhudhuria, kama itakavyoamuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Uteuzi wa Naibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**16.-**(1) Kutakuwa na Naibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye atateuliwa na Rais na ambaye atakuwa msaidizi mkuu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(2) Naibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuwa Afisa Masuuli wa Afisi.

(3) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Naibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ikiwa mtu huyo ana sifa sawa na weledi wa kuteuliwa kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(4) Naibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yake, atakula kiapo mbele ya Rais.

(5) Naibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kuondolewa madarakani endapo atashindwa kutekeleza majukumu yake, kukiuka maadili au kukosa weledi.

Wakaguzi.

**17.-**(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011, kutakuwa na wakaguzi watakaoajiriwa kufanya kazi katika Afisi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar, Nam. 7 ya 2022, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa kushauriana na Bodi, ataamua sifa za msingi, sifa za kitaaluma, uzoefu na weledi kwa ajili ya wakaguzi waliotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(3) Mkaguzi atatekeleza kazi zake kwa mujibu wa Kanuni za Maadili na Utendaji zilizotungwa chini ya Sheria hii na kwa kuzingatia maelekezo yoyote yatakayotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(4) Bodi, kila baada ya muda, itawapandisha madaraja Wakaguzi ambao wana sifa za kupewa madaraja kwa mujibu wa Muundo wa Utumishi wa Afisi ulioandaliwa na Bodi.

(5) Mkaguzi anayefanya kazi katika Afisi hatohamishwa kwenda kwenye taasisi yoyote ya umma bila ya idhini ya Bodi.

(6) Kila Mkaguzi, kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yake atakula kiapo cha kutunza siri kilichoainishwa katika kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

Uajiri wa wafanyakazi wengine.

**18.-**(1) Kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011, Bodi inaweza, kutokana na mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuajiri wafanyakazi wengine kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi za Afisi.

(2) Wafanyakazi wa Afisi wataajiriwa kwa kuzingatia misingi iliyowekwa chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011 na kwa mujibu wa muundo wa utumishi wa Afisi.

(3) Kila mfanyakazi aliyeajiriwa na Afisi, kabla ya kuanza kutekeleza kazi zake, atakula kiapo kwa namna kama ilivyoainishwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

Kuazimwa maafisa.

**19.-**(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, anaweza kuazima afisa yeyote kutoka taasisi yoyote ya umma kama itakavyohitajika, kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi za Afisi.

(2) Afisa wa umma aliyeazimwa na Afisi, wakati wa kipindi cha kuazimwa, atachukuliwa kuwa ni afisa wa Afisi.

(3) Afisa wa umma aliyeazimwa na Afisi kutoka taasisi ya umma hatofanya ukaguzi kwa taasisi hiyo ya umma kwa kipindi cha miezi ishirini na nne ya kwanza ya muda wa kuazimwa.

(4) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza, baada ya kupokea ombi la taasisi ya umma, kumuazima mfanyakazi wake ambaye, kwa kipindi cha kuazimwa huko atakuwa katika maelekezo na usimamizi wa taasisi ya umma aliyoazimwa na afisa huyo hatofanya ukaguzi wa taasisi hiyo ya umma kwa kipindi cha miezi ishirini na nne baada ya kumalizika muda wa kuazimwa.

Huduma za ukaguzi kutoka nje ya Afisi.

**20.-**(1) Kwa madhumuni ya kutekeleza kazi zake, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kupata huduma za ukaguzi kutoka katika taasisi za nje za ukaguzi zilizosajiliwa na Taasisi ya Wahasibu,

Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi au Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi, ambayo washirika wake, wamiliki, wakurugenzi au wafanyakazi wake si waajiriwa wa Afisi au taasisi ya umma kwa ajili ya kusaidia katika ukaguzi.

(2) Taasisi iliyoteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki:

(a) itakasimiwa uwezo wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na uchunguzi na ukaguzi;

(b) itazingatia maelekezo yoyote itakayopewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na itawasilisha ripoti kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na

(c) haitathibitisha matokeo ya uchunguzi au ukaguzi na haitawasilisha ripoti inayotakiwa chini ya Sheria hii isipokuwa ripoti iliyoidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(3) Katika kipindi cha utekelezaji wa kazi chini ya kifungu hiki, wafanyakazi wa taasisi ya nje iliyopewa kazi watafuata masharti ya Sheria hii, Kanuni za Maadili na Utendaji na kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii zinazohusiana na ukaguzi.

(4) Afisa ambaye kabla alikuwa akifanya kazi kama mkaguzi katika taasisi ambayo inakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hatokagua taasisi hiyo isipokuwa baada ya miezi ishirini na nne kutoka muda alioacha kufanya kazi katika taasisi hiyo.

(5) Utoaji wa huduma za ukaguzi zozote kutoka nje ya Afisi chini ya kifungu hiki hautamzuia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutekeleza jukumu lolote kuhusiana na utekelezaji wa uwezo wake.

Kupata huduma ya ushauri wa kitaalamu na ushauri elekezi.

**21.** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, katika kutekeleza majukumu na kazi zake, anaweza kupata huduma au kufanya kazi kwa kushirikiana na wataalamu au washauri elekezi, ikiwa kutoka utumishi wa umma au vyenginevyo, kwa madhumuni ya kuimarisha utendaji wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuzingatia vigezo na masharti kama watakavyokubaliana.

Wajibu wa Maafisa.

**22.-**(1) Maafisa wa Afisi watakuwa na sifa za kitaaluma na ujuzi wa kazi za ukaguzi wanazozifanya, na afisa hatotakiwa:

(a) kushiriki katika ukaguzi au kushughulikia masuala ya ukaguzi akiwa na maslahi kwa Mkaguliwa au masuala mengine; na

(b) kutoa taarifa yoyote ambayo inahusiana na siri ya biashara ya Mkaguliwa ambayo atazijua wakati wa ukaguzi.

(2) Kila afisa wa Afisi atazingatia Kanuni za Maadili na Utendaji zilizotungwa chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA NNE
## BODI YA UTUMISHI YA AFISI

Uanzishwaji na Muundo wa Bodi.

**23.-**(1) Kunaanzishwa Bodi itakayojulikana kama Bodi ya Utumishi ya Afisi ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) mjumbe mmoja kutoka Tume ya Utumishi Serikalini ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti;

(c) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(d) Mwanasheria wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu; na

(e) wajumbe wengine watatu.

(2) Wajumbe waliotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1)(b),(d) na (e) cha kifungu hiki, watateuliwa na Waziri baada ya kushauriana na taasisi husika kwa kuzingatia jinsia, elimu, ujuzi na uzoefu.

(3) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi endapo mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza ya uhasibu, fedha, uchumi au utawala; na

(b) uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba katika masuala ya ukaguzi, fedha, uchumi au utawala; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

Katibu wa Bodi.

**24.-**(1) Bodi itamteua mfanyakazi wa Afisi kuwa Katibu wa Bodi.

(2) Mfanyakazi atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Katibu wa Bodi endapo atakuwa na:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani ya sheria kutoka katika taasisi yoyote inayotambulika na Serikali au ana sifa ya kuwa katibu wa shirika; na

(b) uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano katika utumishi wa umma.

(3) Katibu atawajibika kwa Bodi na:

(a) ataandaa ajenda za vikao vya Bodi kwa kushauriana na Mwenyekiti;

(b) atachukua kwa usahihi kumbukumbu za vikao vya Bodi;

(c) atatunza na kuhifadhi vyema taarifa sahihi na zenye kujitosheleza za Bodi;

(d) atatoa taarifa za vikao vya Bodi kwa wajumbe;

(e) atatoa ushauri kwa Bodi pale unapohitajika; na

(f) atafanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Bodi kwa mujibu wa sheria.

Kazi za Bodi.

**25.** Bodi itakuwa na kazi ya:

(a) kuajiri wafanyakazi wa Afisi;

(b) kuwapandisha madaraja wakaguzi waliyoidhinishwa na wafanyakazi wengine wa Afisi;

(c) kusimamia, kuratibu na kuidhinisha masuala yote ya wafanyakazi;

(d) kusimamia maadili na nidhamu;

(e) kusitisha ajira kwa wafanyakazi wanaofanya kazi kwa mikataba;

(f) kupanga viwango vya mishahara, posho na maslahi mengine kwa wafanyakazi wa Afisi;

(g) kusikiliza na kuamua rufaa zinazohusiana na hatua za kinidhamu;

(h) kuanzisha na kufanya mapitio muundo wa utumishi wa Afisi; na

(i) kufanya jambo jengine lolote ambalo ni muhimu katika utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii.

Mwenendo wa Bodi.

**26.-**(1) Masharti yanayohusiana na mwenendo wa Bodi yatakuwa kama yalivyoainishwa katika Jadweli la Sheria hii.

(2) Waziri anaweza, kwa amri iliyotagazwa katika Gazeti Rasmi,kurekebisha Jadweli chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA TANO
## UKAGUZI NA AINA ZA UKAGUZI

### (a) Ukaguzi

Viwango vya Ukaguzi na Kanuni za Maadili na Utendaji.

**27.-**(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kutekeleza kazi na majukumu yake, ataweka viwango vya ukaguzi vinavyoweza kutumika na ataandaa Kanuni za Maadili na Utendaji maalumu kwa ukaguzi unaofanywa na Afisi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kuongozwa na Vigezo vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Hesabu au vigezo vyengine vya ukaguzi kama atakavyoona inafaa.

(3) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atazingatia mazingira yote, ikijumuisha:

(a) utaratibu mzuri wa ukaguzi unaofaa; na

(b) taaluma ya ukaguzi iendane na vigezo hivyo.

(4) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali:

(a) atafanya maamuzi tofauti juu ya mambo yaliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, kwa aina tofauti za ukaguzi kwa kuzingatia utaratibu mzuri wa ukaguzi unaotambulika; au

(b) kutoa maelekezo maalumu juu ya mambo hayo katika kila suala lolote husika.

Uwasilishaji wa taarifa za fedha.

**28.-**(1) Afisa Masuuli wa taasisi ya umma atawasilisha taarifa za fedha za taasisi yake kwa kuzingatia utaratibu kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016.

(2) Taarifa za fedha zilizowasilishwa na Mkaguliwa ambazo zinahusiani na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016, zitawasilishwa ndani ya kipindi na kwa namna, ikijumuisha taarifa zinazoendana na masharti yoyote yaliyoelezwa na:

(a) sheria yoyote inayotumika kwa Mkaguliwa; au

(b) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ikiwa hakuna sheria hiyo.

Ulinzi wa taarifa.

**29.-**(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atachukua hatua stahiki za tahadhari ya ulinzi dhidi ya utoaji wa siri au taarifa zisizotakiwa kutolewa zilizopatikana kwa mujibu wa kifungu cha 15 ya Sheria hii.

(2) Hatua zilizochukuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, haziwezi kuzuia utoaji wa matokeo yoyote ya ukaguzi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mkaguzi aliyeidhinishwa kuhusiana na matumizi yasiyoidhinishwa, matumizi yasiyofuata taratibu au matumizi yasiokuwa na tija na hasara ambayo yanapaswa kukaguliwa au ukiukwaji wowote au matendo ya kijinai yanayohusiana na masuala ya fedha za Mkaguliwa, lakini utoaji huo wa taarifa unaweza usihusishe ukweli wa utoaji wa taarifa ambao utaathiri maslahi ya umma.

(3) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, mkaguzi aliyeidhinishwa, msaidizi au mtu mwengine anayefanya kazi ya ukaguzi chini ya masharti ya Sheria hii, ana uwezo lakini halazimiki kutoa taarifa aliyoipata katika utekelezaji wa majukumu yake ya kazi katika shauri la kisheria ambalo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali si muhusika.

(4) Masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, hayatotumika katika shauri lolote mbele ya:

(a) Baraza la Wawakilishi au kamati zake; au

(b) Mahakama katika mashauri ya jinai.

Upeo wa ukaguzi.

**30.** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataamua upeo na namna ya uchunguzi au ukaguzi wa hesabu au ukaguzi mwengine wowote wa kila Mkaguliwa, kama ambavyo ataona inafaa katika kutekeleza majukumu na kazi zake.

Ukaguzi wa fedha za umma katika taasisi binafsi.

**31.** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kuhoji, kuchunguza na kuripoti, kama atakavyoona ni muhimu,katika matumizi ya fedha za umma, fedha ya utangulizi au dhamana kwa taasisi binafsi.

Matumizi ya Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani.

**32.** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuwa na uwezo wa kupata ripoti yoyote ya Mkaguzi wa Ndani wa Taasisi za Umma na ripoti nyengine za taasisi ambazo zinapaswa kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ada ya ukaguzi.

**33.-**(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kutoza ada kwa ajili ya ukaguzi wa hesabu za Mkaguliwa, ikizingatiwa kwamba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mwakilishi wake atazingatia:

(a) uhalisia na kiwango cha huduma kilichotolewa;

(b) vigezo vya ukaguzi;

(c) sifa na uzoefu wa watu ambao ni muhimu kuwashirikisha katika utoaji wa huduma hizo;

(d) mambo mengine yoyote ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakavyoona inafaa.

(2) Masharti ya kifungu hiki hayatatumika kwa hesabu za Serikali Kuu na mamlaka za Serikali za Mitaa.

(3) Mkaguliwa atalipa ada ya ukaguzi kwa mujibu wa vigezo na masharti kama itakavyokua katika mkataba au barua ya makubaliano.

Ukaguzi wa awali wa mafao ya kustaafu na fidia.

**34.** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atafanya ukaguzi wa awali wa malipo ya kustaafu na malipo ya fidia ili kuhakikisha kwamba uamuzi na malipo yanayopendekezwa yanafanywa kwa mujibu wa sheria.

Hesabu za Mahakama.

**35.-**(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atachunguza hesabu za Mahakama na vitabu, kumbukumbu na nyaraka nyengine zinazohusika zinazotunzwa au kuwa chini ya usimamizi wa Mahakama.

(2) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atajiridhisha kuwa ada, faini na utekelezaji wa adhabu zote zinazotozwa na Mahakama zinakusanywa ipasavyo na kuingizwa katika hesabu kwa wakati.

Ripoti ya Usimamizi wa Mali.

**36.** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atachunguza ripoti za usimamizi wa mali na anaweza kuomba taarifa na maelezo ya ziada kutoka kwa Msajili wa Hazina ili kumuwezesha kutoa maoni juu ya uhalisia wa hesabu za mali.

**(b) Aina za Ukaguzi**

Ukaguzi wa Kawaida.

**37.** Ukaguzi wa kawaida unaofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali utajumuisha tathmini na uchunguzi wa:

(a) taarifa za fedha na kumbukumbu muhimu;

(b) mfumo wa udhibiti wa ndani na njia nyengine za ukaguzi;

(c) taratibu na njia za ununuzi wa mali za umma;

(d) kufuatwa kwa sheria, kanuni na sera zinazotumika; na

(e) jambo lolote ambalo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakaloona ni muhimu.

Ukaguzi wa Ufanisi.

**38.** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atafanya ukaguzi wa ufanisi kwa kuchunguza matumizi sahihi, tija na ufanisi wa matumizi ya rasilimali za taasisi, kuhoji, kuchunguza na kutoa taarifa kuhusiana na:

(a) matumizi ya fedha na rasilimali kwa taasisi za umma;

(b) mwenendo na utekelezaji wa kazi kwa Maafisa Masuuli, Wakuu na Watendaji Wakuu wa taasisi zote za umma;

(c) kufuatwa kwa sheria za mazingira, kanuni na sera za ndani za mazingira na viwango; au

(d) shughuli nyengine yoyote iliyofanywa na taasisi hizo za umm

Ukaguzi wa uchunguzi.

**39.** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kufanya ukaguzi wa uchunguzi endapo anashuku kuwepo kwa udanganyifu au makosa yanayohusiana na hayo na haraka iwezekanavyo, ataripoti jambo hilo kwa taasisi husika.

Ukaguzi wa Mifumo.

**40.-**(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atafanya ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma.

(2) Ukaguzi chini ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, utalenga katika kuhakikisha kwamba maendeleo, utekelezaji, usaidizi na utunzaji wa teknolojia ya habari au mifumo ya habari inafikia malengo ya biashara, uhifadhi wa taarifa za mali, unaendeleza usiri, uadilifu na upatikanaji wa taarifa zinazohusiana na Mkaguliwa kwa mujibu wa sera za TEHAMA za kitaifa na kimataifa zinazotumika, kanuni, viwango na muundo wa udhibiti.

(3) Endapo taarifa za hesabu na taarifa nyengine zimehifadhiwa katika kompyuta, Afisa Masuuli wa taasisi husika, atahakikisha kwamba, hesabu, kumbukumbu au mambo yanayohitajika yanapatikana kwa maandishi au vyenginevyo, kutoa waraka utakaoonesha kwa usahihi taarifa kamili au sehemu ya taarifa zinazohitajika.

(4) Endapo Mkaguzi anahitaji kupata taarifa na taarifa zimedhibitiwa katika mfumo kwa neno la siri, afisa mwenye dhamana ataruhusu taarifa hizo zipatikane kwa kuweka neno la siri kwa siri bila ya kumuonesha Mkaguzi neno la siri.

(5) Mkaguzi anaweza kunakili taarifa au maelezo yaliyohifadhiwa kieletroniki kwa lengo la kukamilisha jukumu la kazi hiyo.

Ukaguzi mwengine.

**41.-**(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kufanya ukaguzi wa aina nyengine yoyote kama atakavyoona inafaa.

(2) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali anaweza, kwa ombi la mtu yeyote, taasisi ya umma au taasisi nyengine yoyote kufanya ukaguzi maalum au ukaguzi wa aina nyengine yoyote kwa mujibu wa hadidu rejea na masharti mengine aliyoyakubali Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali.

## SEHEMU YA SITA
## UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA NA MAMLAKA NYENGINEZO

Mashirika ya umma na mamlaka nyenginezo.

**42.-**(1) Kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016, ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kila mwisho wa mwaka wa fedha, kila taasisi au shirika la umma litatayarisha na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi taarifa za fedha kwa mujibu wa Vigezo vya Kimataifa vya Utoaji wa Taarifa za Kifedha au Vigezo vya Kimataifa vya Uhasibu vya Sekta za Umma.

(2) Shirika la umma au taasisi itajumuisha mamlaka au chombo chengine:

(a) kilichoanzishwa na sheria au hati nyengine ambapo kinapokea mchango kutoka, au uendeshaji wa shughuli zake, chini ya sheria au hati inayohusiana na hiyo, kuunda au kuanzisha wajibu juu ya mfuko wa umma;

(b) ambacho Serikali imewekeza fedha zake;

(c) kinachosimamia mradi wa Serikali ambayo Serikali ya kigeni, taasisi au taasisi za kimataifa zinachangia fedha, bidhaa au

huduma, iwe zimetolewa au hazijatolewa mahsusi katika mkataba kwa ajili ya mradi unaowajibika kwa fedha za umma zitapaswa kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(d) ambacho hesabu zake zinatakiwa zikaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa sheria;

(e) ambacho Serikali ina hisa nyingi; na

(f) ambacho katika kila mwaka wake wa fedha, kinapokea zaidi ya nusu ya mapato kutoka katika fedha za umma.

Ukaguzi wa mashirika ya umma na mamlaka nyenginezo.

**43.-**(1) Katika kutekeleza majukumu na kazi zake chini ya Sehemu hii, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuwa na uwezo sawa kuhusiana na fedha, stempu, usalama wa mali, ghala na mali nyengine za vyombo vilivyoelezwa chini ya Sheria hii.

(2) Bila ya kujali chochote kilichoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, taasisi au mamlaka inayosimamiwa, itawasilisha taarifa za fedha ndani ya muda kama ilivyoelezwa katika matakwa yao ya udhibiti au masharti ya uanzishwaji wake.

(3) Msajili wa Hazina atawasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali taarifa ya mwaka ya ukaguzi wa chombo ambacho Serikali inamiliki hisa ndogo kwa mapitio na ushauri kwa Serikali.

(4) Baada ya kupokea taarifa za fedha zilizoelezwa katika kifungu cha 42 cha Sheria hii, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali atakagua na atawasilisha ripoti ndani ya kipindi cha miezi sita.

Kuteuliwa kufanya ukaguzi.

**44.-**(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kumruhusu mtu mwenye sifa kufanya uchunguzi, kuhoji au ukaguzi wa vitabu vyote vya hesabu na fedha za taasisi yoyote ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anahitajika kukagua kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, na mtu huyo aliyeruhusiwa atafanya ukaguzi na kuwasilisha ripoti kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa utaratibu ambao Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakavyoelekeza.

(2) Mtu aliyeidhinishwa kufanya kazi za ukaguzi chini ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, atawajibika kufuata masharti yaliyoelezwa katika kifungu cha 17 cha Sheria hii.

(3) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, maoni ya ukaguzi yatabaki kuwa ni majukumu pekee ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

## SEHEMU YA SABA
## RIPOTI YA UKAGUZI

Ripoti ya Ukaguzi ya Mwaka.

**45.-**(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baada ya kupokea taarifa za hesabu zilizoelezwa katika sheria husika, atakagua na kuchunguza hesabu hizo ndani ya kipindi cha miezi sita au kwa kipindi cha zaidi ya hapo kama Baraza la Wawakilishi litakavyoamua kwa azimio baada ya mwisho wa mwaka wa taarifa za hesabu zinazohusika:

(a) atatoa maoni ya kitaalamu kuhusiana na kila taarifa ya hesabu na matokeo ya uchunguzi na ukaguzi, na atatoa maoni au hitimisho kuhusu:

(i) iwapo taarifa za hesabu za mwaka za Mkaguliwa zimeandaliwa vizuri na vielelezo vyote, hali ya fedha katika tarehe maalum na matokeo ya utendaji na mtiririko wa fedha kwa kipindi kinachoishia cha mwaka wa fedha husika kwa mujibu wa sheria na miongozo ya ufungaji wa hesabu inayotumika;

(ii) Mkaguliwa ametekeleza sheria inayotumika kuhusiana na masuala ya fedha, usimamizi wa fedha na mambo mengine yanayohusiana na hayo; na

(iii) taarifa zilizowasilishwa kuhusiana na utekelezaji wa Mkaguliwa
dhidi ya malengo yaliyowekwa; na

(b) kutayarisha ripoti juu ya uchunguzi na ukaguzi wa hesabu zote.

(2) Pamoja na hayo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kutoa taarifa kama rasilimali za Mkaguliwa zimepatikana kwa kuzingatia tija ya kiuchumi na zimetumika kwa ubora na ufanisi.

Kuwasilisha Ripoti ya Ukaguzi.

**46.-**(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha Ripoti kwa Rais kwa mujibu masharti ya kifungu cha 112(5) cha Katiba.

(2) Ripoti iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itawasilishwa na Waziri katika Baraza la Wawakilishi ndani ya kipindi cha siku saba za kikao kinachofuata cha Baraza la Wawakilishi baada ya kupokea ripoti.

Ripoti Maalum ya Ukaguzi.

**47.-**(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wakati wowote atakavyoona inafaa kwamba jambo lolote linalohusiana na fedha au mali za umma kutolewa na kujulikana na Baraza la Wawakilishi, bila ya kuchelewa ataandaa ripoti maalum ya ukaguzi juu ya jambo hilo na atawasilisha ripoti kwa Rais.

(2) Masharti yaliyomo katika kifungu cha 112(5) cha Katiba, yatatumika katika uwasilishaji wa ripoti chini ya kifungu hiki.

Hoja za ukaguzi na yaliyobainika.

**48.-**(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, katika ukaguzi alioufanya au uliofanywa kwa niaba yake, kama kutatokea hoja yoyote au yaliyobainika, atawasilisha hoja hizo na yaliyobainika kwa Afisa Masuuli wa taasisi husika.

(2) Hoja za ukaguzi na yaliyobainika yatatolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Taratibu za Ukaguzi zilizotungwa chini ya Sheria hii.

Ripoti za ukaguzi za Mashirika ya Umma na Vyombo vyengine.

**49.-**(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atatayarisha ripoti ya ukaguzi wa hesabu alizozikagua zilizoelezwa katika Sehemu hii na atawasilisha kwa uongozi wa shirika au chombo chengine kilichokaguliwa ili kutoa majibu na maoni.

(2) Baada ya kupokea yaliyobainika kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Afisa Masuuli wa shirika la umma iliyokaguliwa au chombo hicho, atajibu hoja zilizotolewa ndani ya siku kumi na nne.

(3) Ripoti ya mwisho itakayotolewa kulingana na kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, itawasilishwa na Waziri katika Baraza la Wawakilishi.

Kamati za Uchunguzi za Baraza la Wawakilishi.

**50.-**(1) Kamati ya Uchunguzi wa Hesabu za Serikali Kuu, Kamati ya Uchunguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika au Kamati nyengine yoyote ya Baraza la Wawakilishi zitajadili Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Ripoti Kuu iliyotajwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki baada ya kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi.

(2) Kwa madhumuni ya kutayarisha Ripoti Kuu iliyotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki:

(a) maafisa masuuli watatayarisha mpango kazi wa kuzishughulikia hoja za ukaguzi na kuwasilisha kwa Waziri anayehusika na fedha ;

(b) Waziri anayehusika na fedha ataandaa Ripoti Kuu ya majibu na mpango kazi aliyopokea chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki na:

(i) atawasilisha Ripoti Kuu ya majibu na mipango kazi katika Baraza la Wawakilishi; na

(ii) atawasilisha nakala ya Ripoti Kuu hiyo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ripoti kuwa nyaraka ya umma.

**51.** Ripoti zote za ukaguzi zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zitakuwa nyaraka za umma baada ya kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi.

Utekelezaji wa Ripoti za Ukaguzi.

**52.** Katika kutayarisha Ripoti ya Mwaka ya Ukaguzi, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atajumuisha hali ya utekelezaji wa mipango kazi iliyotayarishwa na Afisa Masuuli na Ripoti iliyojumuishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

**53.** Endapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataamua kutumia vyombo vya habari kutangaza ripoti chini ya Sheria hii, atazingatia mambo yafuatayo:

Matumizi ya vyombo vya habari kutangaza Ripoti.

(a) mtazamo wa jumla wa ripoti au waraka;
(b) namna na mahali itakapotangazwa, itakapopatikana na kusomwa na wananchi;

(c) mahitaji ya kutayarisha muhtasari wa kutangaza ripoti; na

(d) kutumia majukwaa mengine ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakayoona inafaa.

**54.** Wananchi watakuwa na haki ya kupata ripoti za ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya kuweka uwazi na uwajibikaji isipokuwa kama taarifa inayohitajika itahatarisha usalama wa nchi.

Haki ya kupata ripoti za ukaguzi.

**SEHEMU YA NANE**
**MASHARTI YA FEDHA**

**55.** Fedha za Afisi zitajumuisha:

Vyanzo vya Fedha vya Afisi.

(a) fedha zilizoainishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) fedha au mali za Afisi zitakazopatikana kutokana na utekelezaji wa kazi za Afisi chini ya Sheria hii;

(c) malipo ya ada ya ukaguzi na malipo mengine; na

(d) fedha nyengine zozote halali zitakazopokelewa na Afisi.

**56.** Afisi inaweza kufungua hesabu moja au zaidi ya benki kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016.

Hesabu za Benki.

**57.-**(1) Afisa Masuuli wa Afisi atatayarisha makadirio ya bajeti ya mapato na matumizi ya mwaka na mpango kazi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Bajeti ya Afisi.

(2) Afisa Masuuli wa Afisi baada ya kuandaa makadirio ya mapato na matumizi, atawasilisha kwa Waziri si zaidi ya tarehe 31 Machi, ya kila mwaka kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016.

**58.-**(1) Hesabu za Afisi zitakaguliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016.

Ukaguzi wa Hesabu.

(2) Malipo ya ukaguzi wa hesabu za Afisi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki yatalipwa kutoka katika fedha za Afisi.

**59.** Ripoti ya ukaguzi wa hesabu ya Afisi itawasilishwa na kujadiliwa na Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa sheria inayohusika.

Kujadili Ripoti ya ukaguzi wa hesabu za Afisi.

## SEHEMU YA TISA
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa kwa Maafisa wa Afisi.

**60.** Afisa au mfanyakazi yeyote wa Afisi ambaye:

(a) atashiriki katika vitendo vya rushwa;

(b) kwa makusudi anaficha taarifa kuhusu matokeo ya ukaguzi kwa sababu zozote zile kwa lengo la kufaidika kifedha kwa Afisa au mshiriki au mtu mwengine;

(c) kwa makusudi anashindwa kutoa taarifa za ukaguzi unaohusu udanganyifu au kitendo cha rushwa kwa taasisi iliyokaguliwa;

(d) anashindwa kutoa taarifa ya mgongano wa maslahi katika jambo lolote katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii; au

(e) kwa makusudi anatoa, anachapisha au anaitangaza ripoti ya ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au yaliyomo kwa mtu wa tatu ikiwemo vyombo vya habari kabla ya ripoti hiyo kukamilishwa na kuwasilisha rasmi katika Baraza la Wawakilishi na kutolewa nakala kwa taasisi iliyokaguliwa na afisi zilizoidhinishwa,

ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote mbili faini na kifungo.

Makosa kwa wanaokaguliwa.

**61.** Mtu ambaye:

(a) bila ya sababu ya msingi au sababu ya kisheria, atamzuia au kumkwamisha, kumshambulia au kumtisha mfanyakazi wa Afisi au mtaalamu anayefanyakazi chini ya Sheria hii;

(b) bila ya sababu atashindwa kutoa taarifa inayohitajika chini ya Sheria hii;

(c) bila ya sababu atashindwa kutoa taarifa ndani ya muda unaohitajika chini ya Sheria hii;

(d) atatoa taarifa ya uongo au ya kupotosha;

(e) atamdanganya au kwa makusudi atampotosha afisa yeyote wa Afisi anapofanya kazi zake chini ya Sheria hii; au

(f) kuingilia kati au kwa kumpa shindikizo mfanyakazi yeyote wa Afisi au mtu yeyote aliyeidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya kazi zake chini ya Sheria hii,

ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano za Kitanzania au kifungo kisichozidi miaka miwili au adhabu zote mbili ya faini na kifungo kwa pamoja.

## SEHEMU YA KUMI
## MASHARTI MENGINEYO

Matumizi yasiofuata utaratibu, yasiyo na tija na ya upotevu.

**62.-**(1) Bila ya kuzingatia mipaka ya dhima chini ya sheria yoyote:

(a) Afisa Masuuli atawajibika kwa kufanya matumizi kinyume na Sheria, matumizi yasiyo na tija na ya upotevu kwa makusudi au kwa uzembe uliofanywa au kuidhinishwa na yeye, kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki; na

(b) mfanyakazi yeyote ambaye kwa makusudi au kwa uzembe ameingia au ameidhinisha matumizi yasiyofuata utaratibu au yasiyokuwa na tija au ya upotevu atawajibika kwa matumizi hayo.

(2) Endapo Afisa Masuuli atafahamu kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amefanya uamuzi ambao ukitekelezwa utapelekea matumizi yasiyofuata utaratibu, yasiyo na tija na upotevu, Afisa Masuuli huyo hatawajibika kwa matokeo ya matumizi yasiyofuata utaratibu, yasiyo na tija na upotevu kwa baadae iwapo kwamba Afisa Masuuli huyo amemtaarifu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa maandishi kuwa matumizi hayo yatapelekea ukiukwaji wa sheria na hayatakua na tija na yatakuwa ni ya upotevu.

(3) Uamuzi wowote wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa kuendelea na utekelezaji wa uamuzi chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, na sababu za uamuzi huo, utakuwa kwa maandishi, na Afisa Masuuli haraka atamtaarifu mkaguzi wa nje na chombo cha usimamizi.

(4) Afisa Masuuli haraka iwezekanavyo atamtaarifu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa maandishi, kwamba:

(a) matumizi yasiyofuata utaratibu, yasiyo na tija na ya upotevu yaliyofanywa na uongozi wa taasisi ya umma;

(b) iwapo mtu yeyote anayehusika au yupo chini ya uchunguzi kwa matumizi yasiyofuata utaratibu, yasiyo na tija na upotevu; na

(c) hatua ambazo zimechukuliwa:

(i) kurejesha au kusahihisha matumizi hayo; na

(ii) kuzuia kutokea tena matumizi hayo.

Hatua za kiutawala.

**63.** Mfanyakazi yeyote wa Afisi au mtu wa nje aliyeidhinishwa kufanya kazi na Afisi ambaye itathibitika kuwa amekiuka maadili, amepokea hongo au rushwa kwa namna yoyote ili kuficha udanganyifu au kitendo cha rushwa kutoka kwa Mkaguliwa, atawajibika kuchukuliwa hatua za kiutawala kwa kuzingatia masharti ya Sheria Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011 au sheria nyengine yoyote.

Kutoa taarifa ya udanganyifu na rushwa.

**64.** Wafanyakazi wote wa Afisi au waliopewa kazi na Afisi watawajibika kufichua udanganyifu au rushwa mara tu watakapobaini na hatua za nidhamu zitachukuliwa dhidi ya afisa anatakayeficha siri za udanganyifu au rushwa.

Kutangaza mgongano wa maslahi.

**65.-**(1) Afisa wa Afisi ambaye ana mgongano wa maslahi kwa jambo lolote kwa Mkaguliwa atatoa taarifa kwa maandishi, aina ya mgongano wa maslahi na hatoshiriki katika ukaguzi unaohusiana na Mkaguliwa.

(2) Afisa ambaye atashindwa kubainisha mgongano wa maslahi wa jambo lolote kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atachukuliwa hatua za kiutawala.

Mtoa taarifa.

**66.-**(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataweka utaratibu wa kupokea taarifa za siri za watumishi wa Afisi wanaofanya vitendo kinyume na sheria au maagizo ya ukiukwaji wa sheria zinazohusu fedha za umma, upotevu mkubwa, uongozi usioridhisha na matumizi mabaya ya afisi.

(2) Mtu yeyote anayetoa taarifa za rushwa au ukosefu wa maadili ya mkaguzi iwapo ana uhakika wa taarifa au kwa nia njema au anaamini tuhuma au taarifa zake ni sahihi, atahifadhiwa.

(3) Madai na mambo yanayotolewa kwa siri yatapitiwa na kuzingatiwa ipasavyo na baadhi ya mambo yatakayozingatiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ikiwemo uzito wa madai, ukweli wake na kiwango cha madai hayo yatathibitishwa au kulinganishwa na vyanzo vyengine vya taarifa.

(4) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hatofichua utambulisho wa mtu chini ya kifungu hiki isipokuwa:

(a) mtu huyo amekubali kutajwa;

(b) utambulisho wake ni muhimu kuwezesha taasisi za utekelezaji sheria kuchunguza au kutoa taarifa iliyofichuliwa;

(c) itahitajika kisheria endapo tuhuma za uongo zimetolewa; au

(d) mtuhumiwa anastahiki kupewa taarifa ikiwa ni haki yake kisheria na katika mazingira hayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atamjulisha mtoa taarifa za siri kabla ya kumtambulisha.

Kinga dhidi ya hatua za kisheria.

**67.** Hakuna hatua au taratibu nyengine zitakazochukuliwa dhidi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu mwengine aliyeajiriwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akiwa kama mkaguzi aliyeidhinishwa au Afisa, taasisi ya ukaguzi au mtaalamu

au kwa cheo chochote kuhusiana na utekelezaji wa kazi, majukumu, uwezo au haki ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali chini ya Sheria hii au sheria nyengine zinazotumika Zanzibar kwa masharti kwamba amefanya hivyo kwa nia njema.

Kanuni.

**68.** Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Kufuta na Kubakiza.

**69.-**(1) Sheria ya Kuanzisha Sheria ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam. 11 ya 2003 inafutwa.

(2) Bila ya kujali ufutaji chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa au lililokusudiwa kufanywa chini ya Sheria iliyofutwa itachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

**JADWELI**

**MWENENDO WA BODI**

**[Chini ya kifungu cha 26(1)]**

Muda wa wajumbe wa Bodi.

**1.** Isipokuwa mjumbe anayeingia kwa nafasi yake, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Vikao vya Bodi.

**2.-**(1) Bodi itakutana mara moja kila baada ya miezi mitatu katika vikao vyake vya kawaida na inaweza kukutana katika vikao vya dharura muda wowote inapohitajika kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

(2) Vikao vyote vya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti, ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao na endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe watakaokuwepo watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

Akidi ya vikao.

**3.** Akidi katika vikao vya Bodi itakuwa ni zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe wake.

Uamuzi wa Bodi.

**4.** Uamuzi wa Bodi utafanywa kwa makubaliano, ikiwa hakuna makubaliano, uamuzi utafanywa kwa wingi wa kura na ikitokea kura kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

Taratibu za vikao vya Bodi.

**5.** Bila ya kuathiri masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kuandaa taratibu zake zenyewe kuhusiana na vikao na utaratibu wa kutekeleza shughuli zake ikijumuisha Kamati za Bodi.

Mjumbe mualikwa.

**6.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote ambaye si mjumbe wa Bodi kuhudhuria katika majadiliano yoyote ya vikao vya Bodi kama mtaalamu lakini mjumbe mualikwa huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Kumbu-kumbu za vikao vya Bodi.

**7.** Kumbukumbu za mwenendo wa kikao cha Bodi zitathibitishwa na Bodi katika kikao kinachofuata na kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu.

Kubainisha maslahi.

**8.-(**1) Mjumbe wa Bodi ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo juu ya jambo linalohusika au linalotakiwa kujadiliwa na Bodi, haraka iwezekanavyo baada kutambua, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni mwa kikao cha Bodi.

(2) Ubainishaji wa maslahi utawekwa katika kumbukumbu za kikao na Mjumbe aliyebainisha:

(a) hatahudhuria katika majadiliano ya Bodi katika kufanya uamuzi wa jambo hilo; au

(b) hatamshawishi mjumbe mwengine yeyote katika kufanya uamuzi unaohusiana na jambo hilo.

Kusita kuwa mjumbe.

**9.** Mjumbe atasita kushika nafasi yake ikitokea moja kati ya yafuatayo:

(a) amejiuzulu;

(b) ikiwa hatahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya kuwa na sababu za msingi;

(c) ikiwa atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu za afya ya kimwili au kiakili;

(d) kusitishwa na Waziri kwa kushindwa kutimiza matarajio ya Mamlaka;

(e) ikiwa mjumbe atasita kuwa mwakilishi wa taasisi iliyompendekeza Mjumbe huyo; au

(f) kifo.

Bodi kukasimu kazi zake.

**10.-**(1) Bodi inaweza, pale itakapoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au Kamati ya Bodi.

(2) Endapo Bodi itakasimu kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatoa miongozo kwa maandishi endapo itahitajika ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa kazi hizo.

Kamati za Bodi.

**11.** Bodi inaweza kuunda kamati na kuipa kazi maalum kama itakavyoona inafaa.

Posho la wajumbe wa Bodi.

**12.** Wajumbe wa Bodi watastahiki kulipwa posho kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011 na sheria nyenginezo zinazohusika.

## MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni ya Mswada huu ni kufuta Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam. 11 ya 2003 na kutunga Sheria ya Ukaguzi wa Umma na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Pamoja na mambo mengine, Mswada unaelezea uanzishaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi wa Afisi. Katika utekelezaji wa kazi za ukaguzi wa fedha na rasilimali za Serikali, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inapaswa kuzingatia misingi na vigezo vya ukaguzi vya Kitaifa na Kimataifa. Aidha, Afisi inatakiwa kusimamia ipasavyo misingi ya haki na usawa katika matumizi ya rasilimali fedha za Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016 pamoja na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, Nam. 11 ya 2016.

Kwa kuzingatia misingi na masharti ya utawala bora wa kufuata sheria, Mswada umeweka masharti ya kuhakikisha kwamba mipango na bajeti ya Serikali kwa Serikali kuu na taasisi zake zote inatumika kwa utaratibu na kufikia shabaha iliyojiwekea bila ya kwenda kinyume na Sera, Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo. Pia, taasisi nyengine ikiwemo muhimili wa Mahakama na Baraza la Wawakilishi nayo inahakikisha rasilimali za umma zinatumika ipasavyo.
Mswada huu umegawika katika sehemu kumi.

***Sehemu ya Kwanza*** inahusu masharti ya awali ambayo yamejumuisha jina fupi na kuanza kutumika kwa sheria, matumizi ya sheria na kuweka ufafanuzi wa maneno muhimu yaliyotumika katika Mswada huu.

***Sehemu ya Pili*** inaelezea Uanzishwaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ikiwa kama chombo huru kinachojitegemea. Pia, inaeleza kazi za Afisi, pamoja na Muundo wa Utumishi wa Afisi.

***Sehemu ya Tatu*** Sehemu hii inahusu Usimamizi wa Afisi, Mamlaka na uwezo wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. vilevile, sehemu hii inaeleza uwezo wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa mapendekezo na kupata taarifa kwa ajili ya ukaguzi. Aidha, imeeleza uteuzi, kazi na majukumu wa Naibu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Sehemu hii pia imeelezea Uajiri wa wafanyakazi wengine wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Afisi kuwa na uwezo wa kuazima maafisa, kupata huduma za ukaguzi kutoka nje ya Afisi, Kutafuta Ushauri wa kitaalamu na ushauri elekezi, wajibu wa maafisa wa Afisi, na mambo mengine.

***Sehemu ya Nne*** Sehemu hii inahusu Bodi ya Utumishi ya Afisi, Uanzishwaji na muundo wa Bodi, Katibu wa Bodi, Kazi za Bodi na Mwenendo wa Bodi.

***Sehemu ya Tano*** Sehemu hii inaelezea kuhusu Ukaguzi na Aina za Ukaguzi, Viwango vya Ukaguzi na Kanuni za Maadili na Utendaji, Uwasilishaji wa taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi, Ulinzi wa Taarifa, Ukaguzi wa fedha katika Taasisi binafsi, Matumizi ya ripoti ya Mkaguzi wa ndani, Ada ya Ukaguzi, Ukaguzi wa awali wa mafao ya kustaafu na fidia, Hesabu za Mahakama pamoja na Ripoti ya Uhakiki hMali, Ukaguzi wa Uchunguzi, Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA na Ukaguzi mwengine.

***Sehemu ya Sita*** Sehemu hii inaelezea Ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Mamlaka Nyenginezo.

***Sehemu ya Saba*** Sehemu hii inaelezea Ripoti ya Ukaguzi ambapo inajumuisha Ripoti ya Ukaguzi ya Mwaka, Ripoti ya Ukaguzi Maalum, Ripoti za ukaguzi za Mashirika ya Umma na vyombo vyengine, Kamati za Uchunguzi za Baraza la Wawakilishi, Ripoti kuwa

nyaraka za Umma, Utekelezaji wa Ripoti za Ukaguzi pamoja na Matumizi ya Vyombo vya Habari kutangaza Ripoti.

***Sehemu ya Nane*** Sehemu hii inaelezea Masharti ya Fedha ikiwemo Vyanzo vya Fedha vya Afisi, Hesabu za Benki, Bajeti ya Afisi, Ukaguzi wa hesabu na kujadili ripoti ya ukaguzi wa hesabu za Afisi.

***Sehemu ya Tisa*** Sehemu hii inahusu Makosa na Adhabu kama vile makosa kwa maafisa wa Afisi na makosa kwa wakaguliwa.

***Sehemu ya Kumi*** Sehemu hii inaelezea Masharti Mengineyo, ikijumuisha matumizi yasiyofuata utaratibu, Hatua za kiutawala, Kutoa taarifa ya udanganyifu na rushwa, Kutangaza mgongano wa maslahi, mtoa taarifa, kinga dhidi ya hatua za kisheria, uwezo wa Waziri kutunga kanuni na Kufuta Sheria Nam. Nam. 11 ya 2003 na kubakiza.

Mwisho lipo Jadweli linaloeleza mwenendo wa Bodi.

**ZANZIBAR**
23Agosti, 2023

**(MHE. HAROUN ALI SULEIMAN)**
WAZIRI WA NCHI, (OR), KATIBA, SHERIA,
UTUMISHI NA UTAWALA BORA